



Australian Government



ParentsNext

# Kuripoti juu ya maendeleo yako



Wakati wa kushiriki katika ParentsNext, unaweza kuhitaji kuripoti juu ya shughuli zako.

Mshauri wako wa ParentsNext atakuambia nini cha kuripoti na siku zako za kuripoti.

Utaulizwa **kuripoti kwa Centrelink na ParentsNext** – unaweza kuripoti kwa simu au kwenye mtandao.

## MHIMU

Ili kuendelea kupata Malipo ya Uzazi ni muhimu kutoa ripoti juu ya siku zilizotajwa na mshauri wako. Usipofanya hivo malipo yako yanaweza kuathiriwa.

Ikiwa kitu kinatokea na huwezi kuhudhuria au kuripoti kwa wakati, mwambie mshauri wako mara moja ili kuepuka malipo yako kuweza kusimamishwa. Unaweza pia kuhitaji kuzungumza na Centrelink.

## Kutoa taarifa mtandaoni

Unaweza kuripoti **Centrelink** kupitia **tovuti ya myGov** au **Express Plus Centrelink** mobile app. Unaweza kuripoti **ParentsNext** kupitia **Job Seeker** app.

Mshauri wako anaweza kukusaidia **kama unahitaji msaada wa kufungua akaunti ya myGov** au kuunganisha apps kweye akaunti yako ya myGov.

### Kutoa taarifa Centrelink

**Ripoti kipato chako** na **kuwa umetimiza matakwa** katika mpango wako.

### Kutoa taarifa ParentsNext

**Thibitisha umehudhuria** shughuli katika Mpango wako wa Ushiriki.

## Vidokezo kwa ParentsNext vya kuripoti shughuli



**Kama huwezi kuripoti mtandaoni**, unaweza kumpigia mshauri wako siku ya kuripoti na watakusaidia kutoa taarifa.



**Unaweza kujiandikisha kuweza kukumbushwa kwa SMS**, kupitia **Job Seeker app**, au kwa barua pepe. Uliza mshauri wako kwa habari zaidi.



**Unaweza kuongeza ahadi zako za familia** kwa kalenda katika **Job Seeker app** au mwambie mshauri wako, ili waweze kupanga shughuli zinazolingana na maisha ya familia yako.

Kwa habari zaidi tembelea [dese.gov.au/parentsnext](https://dese.gov.au/parentsnext)